# BARAZA LA MASOKO YA MITAJI (CMT)
# MFULULIZO WA ELIMU KWA UMMA MTANDAONI

**TAREHE: JUMAMOSI, TAREHE 20 DESEMBA 2025**

Hapa chini ni muundo wa Maelezo ya Maswali na Majibu (Q&A Script) yaliyoundwa kwa ajili ya watu wawili (Mtangazaji/Msimamizi na Mwakilishi wa Baraza (TR)). Maelezo haya yanazingatia kikamilifu Kanuni za Baraza la Masoko ya Mitaji na Dhamana, Tangazo la Serikali Na. 649 ya mwaka 2023.

## Andiko la Instagram Live: Lijue Baraza

**Maudhui:** Ufunguaji wa Rufaa
**Lengo:** Sifa za Mwombaji, Muda, na Nyaraka
**Chanzo cha Mamlaka:** Tangazo la Serikali Na. 649 ya mwaka

## SEHEMU YA 1: UTANGULIZI

**Mtangazaji.** Habari tena, kila mmoja! Karibuni kwenye kipindi chetu cha pili cha mubashara kwa ajili ya Baraza la Masoko ya Mitaji. Mimi ni Stella Anastazi, niko hapa tena na Ademson Emmanuel. Nitakuwa msimamizi wa kipindi cha leo na Emmanuel ndiye mzungumzaji wetu kutoka Barazani.

**Mtangazaji.** Katika kipindi kilichopita, tuliangazia muundo, mamlaka, na uhuru wa Baraza ambapo tulijifunza kuhusu sifa za kuwa mjumbe wa Baraza, uwepo wa sekretarieti, masuala ya mgongano wa maslahi, na nini Baraza linaweza kufanya na nini haliwezi kufanya.

Leo, tunaingia kwenye hatua za utekelezaji. Ikiwa una mgogoro, unaanzaje mchakato? Tutachambua nani anastahili kukata rufaa, muda wa ukomo (deadlines) ambao unapaswa kuujua, na nyaraka zinazohitajika ili shauri lako lisikilizwe.

**Mtangazaji.** Tuuanze mchakato.

## SEHEMU YA 2: MASWALI NA MAJIBU

### 2.0 Nani anaweza kukata rufaa? Je, mimi nastahili?

**Mtangazaji.** Emmanuel, tuseme mtu hafurahishwi au haridhiki na uamuzi uliofanywa na Soko la Hisa au Mamlaka. Je, kila mtu anaweza tu kuingia Barazani na kufungua shauri?

**TR.** Si hivyo hasa. Ili kufungua rufaa, lazima uwe Mtu Aliyeumia/Mwenye Malalamiko (Aggrieved Person). Hii inamaanisha kuwa uamuzi, hatua, au hata kushindwa kuchukua hatua kwa Mamlaka au Soko la Hisa kukuathiri moja kwa moja (Kanuni ya 8). Hususan, hii inajumuisha; (Kanuni ya 7)

- **Watu Wenye Leseni.** Kama vile mawakala (brokers) au washauri wa uwekezaji ambao leseni zao zimekataliwa au kufutwa.
- **Wapatanishi wa Soko.** Taasisi zenye migogoro na Mamlaka au wateja.
- **Kampuni Zilizoorodheshwa.** Kampuni zinazokabiliwa na kuondolewa au kusitishwa kwenye Soko la Hisa.
- **Wawekezaji/Umma.** Kwa mfano, ikiwa una malalamiko ambayo hayajatatuliwa dhidi ya wakala wako, Soko la Hisa au Mamlaka.

Rufaa mbele ya Baraza inaweza kufanywa na mtu mwenyewe au mrufani anaweza kuwakilishwa na mtu aliyesajiliwa kama mpatanishi wa soko, mshauri wa kodi, mhasibu, mkaguzi wa hesabu au wakili.

### 2.1 Je, kuna mamlaka nyingine yoyote ya juu zaidi ya Baraza la Masoko ya Mitaji yenye jukumu la kusikiliza na kuamua mashauri ya masoko ya mitaji?

**TR.** Ndiyo, ipo. Ikiwa upande haujaridhika na maamuzi uliotolewa na Baraza, upande huo unaweza kukata rufaa dhidi ya maamuzi huo kwenda **Mahakama ya Rufani.** Hii ni kwa sababu Baraza ni mamlaka ya juu ya kisheria (superior Tribunal of record) na lina mamlaka sawa na Mahakama Kuu katika masuala ya madai. Upande usioridhika unapaswa kutoa taarifa kwa Baraza ndani ya siku 30 kuhusu nia yake ya kukata rufaa.

Ikumbukwe kuwa rufaa kwenda Mahakama ya Rufani ni kwa ajili ya **hoja za kisheria (points of law)** tu na si hoja za ukweli (points of fact). Hoja ya kisheria hulenga katika sheria inasemaje, inatafsiri sheria na miongozo. Hoja ya ukweli hulenga katika nini kilitokea, inathaminisha ushahidi na maelezo. Rufaa hizi hufanywa kwa mujibu wa Kanuni za Mahakama ya Rufani za mwaka 2019 (Kanuni ya 40 na 41).

### 2.2 Muda wa Ukomo: Saa Inayoyoma

**Mtangazaji.** Muda ni kila kitu katika ulimwengu wa kifedha. Mtu ana muda gani wa kuamua kama akate rufaa au la?

**TR.** Lazima uwe mwepesi sana. Kuna muda wa ukomo wa aina mbili;

- Notisi ya Nia ya Kukata Rufaa (Notice of Intention to Appeal). Lazima uifungue ndani ya siku 7 tangu uamuzi utolewe. Hii hufanywa kupitia Fomu ya CMT Na. 1, na unatakiwa kueleza ikiwa unakata rufaa dhidi ya uamuzi mzima au sehemu tu ya uamuzi (Kanuni ya 9).
- Hati ya Rufaa (Statement of Appeal). Hii lazima ifunguliwe ndani ya siku 30 tangu tarehe ambayo uamuzi wa Mamlaka uliwasilishwa kwako. Hii hufanywa kupitia Fomu ya CMT Na. 2 na iambatane na nyaraka zote muhimu kwa ajili ya uamuzi wa rufaa hiyo (Kanuni ya 8 na 11).

Nyaraka hizi ni pamoja na nakala iliyothibitishwa ya uamuzi wa Mamlaka, nakala iliyothibitishwa ya mwenendo wa shauri (proceedings), nakala ya notisi ya nia ya kukata rufaa, hati ya rufaa na nyaraka nyingine zozote muhimu.

### 2.3 Kukosa Muda wa Ukomo: Je, Kuna Nafasi ya Pili?

**Mtangazaji.** Vipi ikiwa mtu amepitisha kile kipindi cha siku 30? Je, ndiyo case imeisha?

**TR:** Unaweza kuomba Ongezeko la Muda kwa kutumia Fomu ya CMT Na. 5. Hata hivyo, Baraza litakubali ombi hili ikiwa tu linaona ni kwa ajili ya haki na usawa, na baada ya upande mwingine kupewa nafasi ya kusikilizwa. Jambo la muhimu ni kwamba ombi hili la kuongezewa muda lazima lifunguliwe ndani ya siku 7 tangu ukomo wa awali ulipopita (Kanuni ya 14).

### 2.4 Makaratasi: Nyaraka gani zinahitajika?

**Mtangazaji.** Katika kipindi chetu cha kwanza, tulijifunza kuwa kuna Sekretarieti inayoshughulikia utawala. Je, ni nyaraka gani hasa wanazohitaji kutoka kwa mrufani ili kuanza shauri?

**TR.** Ili kuanzisha rufaa rasmi, lazima uwasilishe Hati ya Rufaa (Fomu Na. 2). Lazima yaambatane na;

1. Nakala iliyothibitishwa ya uamuzi unaoukatiwa rufaa.
2. Nakala iliyothibitishwa ya mwenendo wa shauri kutoka Mamlaka (ikiwa inahusika).
3. Nakala ya Notisi ya Nia ya Kukata Rufaa uliyokuwa umeshaifungua.
4. Nyaraka nyingine zozote zinazounga mkono shauri lako.

### 2.5 Gharama: Ada za Kufaili ni kiasi gani?

**Mtangazaji.** Je, Baraza linatoza ada kama mahakama za kawaida? Na kama ndivyo, gharama za kufungua nyaraka hizi zikoje?

TR. Ndiyo, Baraza linatoza ada za kufaili na ada hizo zimeorodheshwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni. Huu hapa ni mchanganuo wa haraka;

- **Notisi ya Nia ya Kukata Rufaa:** TZS 50,000.
- **Kuwasilisha Hati ya Rufaa (Statement of Appeal):** TZS 200,000.
- **Kuwasilisha Hati ya Majibu (Statement of Reply):** TZS 50,000.
- **Kuwasilisha Hati ya Ziada (Additional Statement):** TZS 100,000.
- **Ombi la Utekelezaji wa Tuzo (Execution of Decree):** TZS 30,000.
- **Ombi la Ongezeko la Muda:** TZS 50,000.
- **Ada ya Kupitia Nyaraka (Perusal Fee):** TZS 40,000.
- **Hiari ya kujiunga kama Mrufani-Mwenza (Co-Appellant):** TZS 200,000.
- **Ombi la kutengua uamuzi uliotolewa bila upande mwingine kuwapo (Ex-Parte):** TZS 1,500,000.
- **Taarifa ya kuondoa rufaa:** TZS 3,000,000.
- **Ada ya kupata nakala ya Hukumu, Mwenendo n.k.:** TZS 50,000.

## 2.6 Mchakato: Nini hutokea baada ya kufungua?

**Mtangazaji.** Nikishakabidhi hati yangu ya Rufaa na kulipa ada, nini kinafuata?

**TR.** Msajili anagonga muhuri rufaa yako na kumpa taarifa Mjibu Rufaa (yule unayemlalamikia). Mjibu Rufaa ana siku 14 za kuwasilisha Hati ya Majibu (Statement of Reply) kupitia Fomu CMT Na. 3. Ikiwa usikilizaji wa ana kwa ana (oral hearing) unahitajika, Msajili atapanga tarehe na kuwajulisha wote kupitia Fomu CMT Na. 4(a) (Kanuni ya 12).
Pia, katika hatua hii, upande wowote utakaothiriwa na mwenendo wa shauri una haki ya kujiunga.

**Mtangazaji.** Je, kukata rufaa hii kunasimamisha moja kwa moja maamuzi wa Mamlaka?
**TR.** Kwa kawaida, hapana. Maamuzi wa awali unabaki palepale mpaka Baraza litakapotoa maamuzi wake wa mwisho.

**Mtangazaji.** Je, naweza kubadili mawazo? Vipi kama nataka kurekebisha maelezo yangu au kufuta shauri kabisa?

**TR:** Unaweza kuomba kurekebisha maelezo yako ndani ya siku 7 tangu ombi lako, kwa ada ya TZS 100,000. Pia unaweza kuondoa rufaa wakati wowote kabla ya usikilizaji kuanza kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Msajili. Ila kumbuka, ikiwa muda wa usikilizaji umekaribia, lazima utoe taarifa angalau siku 3 kabla, na ada ya kuondoa rufaa ni TZS 3,000,000 (Kanuni ya 16).

## SEHEMU YA 3: HITIMISHO

**Mtangazaji.** Hiki kimekuwa kikao cha mafunzo sana! Sasa tunajua kuwa wakati milango ya Baraza iko wazi, lazima uwe na fomu sahihi, ulipe ada stahiki na muhimu zaidi, uzingatie muda wa siku 7 na siku 30.

**Mtangazaji.** Asante, Emmanuel, kwa kutufafanulia taratibu hizi. Kwa watazamaji wetu, ikiwa umepitwa na lolote au unahitaji fomu maalum zilizotajwa, tafadhali wasiliana na Baraza kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii, piga simu na utaelekezwa vyema. Pia, jisikie huru kutembelea tovuti ya Baraza; ina fomu na taratibu zote zilizopangwa vizuri. Baraza, kama rafiki wa soko, liko hapa kwa ajili yako, hivyo usiogope kuwasiliana nalo.

**Mtangazaji.** Tunatarajia kukuona katika kikao chetu kijacho ambapo tutajadili Mahudhurio ya Pande za Shauri, Haki za wahusika, uwakilishi na wajibu. Maelezo ya kikao kijacho yatawasiwa kwenu.

**Mtangazaji.** Endelea kupata habari na uendelee kuwekeza! Tunawatakia Heri ya Krismasi na Mwaka Mpya wenye mafanikio.